National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"





## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

# CHUO CHA TAIFA CHA UTALII

Jarida Maalum Toleo Na. 01

# YALIYOMO


01 KUHUSU CHUO

02 UDAHILI

03 MIUNDOMBINU

04 UKARABATI

05 UONGOZI NA UTAWALA BORA

06 WATUMISHI

07 USHIRIKIANO WA KIMKAKATI






# WANAFUNZI WAKISHIRIKI MAFUNZO KWA VITENDO










# DIBAJI



Karibu kwenye Jarida Maalum la Chuo cha Taifa cha Utalii, linaloangazia mafanikio ya Chuo pamoja na hatua kubwa na za kihistoria zilizofikiwa na Chuo chetu kuanzia Agosti 2022 hadi Juni 2024. Katika kipindi hiki tumeshuhudia maendeleo makubwa katika utoaji mafunzo, kuongezeka kwa matumizi teknolojia, uboreshaji wa miundombinu, pamoja na uimarishaji huduma kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla.

Lengo la jarida hili ni kutoa muhtasari wa mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Ushauri, Uongozi wa Chuo, wafanyakazi, wanafunzi,** pamoja na **wadau wetu muhimu**. Tunajivunia hatua hizi ambazo zimeleta mabadiliko chanya na kutupeleka mbele katika safari yetu ya kuwa kituo cha umahili cha mafunzo na utafiti katika sekta ya utalii na ukarimu nchini.

Mafanikio haya ni pamoja na kuanza kwa ujenzi wa jengo la taaluma (Academic Block) katika kampasi ya Arusha, uzinduzi wa viwango vipya vya mishahara (NCT New Salary Scheme), muundo mpya wa taasisi pamoja na ujazaji wa nafasi muhimu za kiutendaji katika taasisi. Katika kipindi hiki Chuo kimefanikiwa kuanzia muundo mpya wa utumishi (Scheme of Service), kuhuisha mkataba wa huduma kwa wateja (Client Service Charter), na kusaini mikataba ya ushirikiano (MOUs) na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

Katika elimu na utafiti, tumefanikiwa kuandaa kongamano la kimataifa la pili na la tatu (2nd and 3rd International Conferences), kuanzisha kituo cha ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi, kuboresha huduma za maktaba na maabara zetu kwa teknolojia za kisasa. Pia, hatuwezi kusahau mafanikio katika kuboresha mazingira ya kujisomea katika kampasi zetu, ikiwemo ukarabati wa Kampasi ya Bustani, utoaji wa huduma bora ya chakula katika mji wa Kiserikaki Mtumba, Dodoma, pamoja na upatikanaji wa ardhi Jiji Mwanza and katika mkoa wa Njombe kwa ajili ya upanuzi wa miradi yetu ya maendeleo.

Mafanikio haya yamewezekana kutokana na juhudi kubwa na ushirikiano na wadau wote husika. Tunawaalika wote kuendelea kushirikiana nasi katika kuendeleza mafanikio haya. Jarida hili ni ushuhuda wa juhudi zetu na dhamira ya kuendelea kuboresha elimu na huduma kwa manufaa ya sekta yetu ya utalii na jamii kwa ujumla.

Tunatumaini kuwa jarida hili litakuwa chachu ya kuhamasisha na kuendeleza juhudi zetu za pamoja katika kuleta mabadiliko chanya na kufikia malengo yetu ya muda mrefu. Kwa niaba ya uongozi wa Chuo natoa shukurani za dhati kwa ushirikiano wenu na karibuni sana kupitia jarida hili ili kupata taarifa za kina kuhusu hatua tulizopiga na mafanikio yaliyopatikana.

**Dr. Florian Mtey, (PhD)**
Mkuu wa Chuo


CHA TAIFA CHA UTALII
MAKAO MAKUU
KAMPASI YA MWANZA
BUSTANI
ARUSHA
MWANZA
TEMEKE

National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# KUHUSU CHUO

Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) ni taasisi ya Umma iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na.30 ya Mwaka 1997. Chuo kimekasimiwa dhamana ya kutoa Mafunzo, Kufanya Tafiti na Kutoa Ushauri wa Kitaalamu katika fani za Ukarimu, Utalii na Uratibu wa Matukio.

Chuo Cha Taifa cha Utalii kina jumla ya Kampasi nne ambazo ni; Temeke (2001), ARUSHA(2008), Bustani (2011) na Mwanza (2020).






MAHAFALI YA CHUO KATIKA UKUMBI WA JNICC

# UDAHILI











Chuo Kimeendelea kushuhudia ongezeko la idadi ya wanafunzi wanojiandikisha katika kozi mbalimbali za Utalii, Ukarimu na Uratibu wa Matukio katika kampasi zetu zote nne (Bustani, Mwanza, Temeke na Arusha. Kwa mwaka wa masomo 2023/2024 Chuo kimepokea jumla ya wanafunzi **1243** ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 204 sawa na ongezeko la asimilia 19.63 ikilinganishwa na mwaka wa masomo 2022/23



MCHORO WA JENGO JIPYA LA TAALUMA KAMPASI YA ARUSHA












National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# MIUNDOMBINU

## UJENZI WA JENGO JIPYA LA TAALUM (ACADEMIC BLOCK) ARUSHA

Chuo kimefanikiwa kuanzisha ujenzi wa jengo jipya (Academic Block) katika Kampasi ya Arusha Septemba 2023. Majengo haya yanajumuisha madarasa ya kisasa, maabara za mafunzo, na ofisi za wakufunzi, ambazo zote kwa pamoja zinalenga kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundisha.

Jengo hili likikamilika litakua na uwezo wa kubeba wanafunzi zaidi ya 2000

## WATUMISHI WA CHUO KATIKA MATUKIO MBALIMBALI










## WATUMISHI




### Mishahara (NCT New Salary Scheme)

Mwezi Disemba 2023, Chuo kilifanikiwa kuanza utekeleza wa viwango vipya vya mishahara ambavyo vimeboresha maslahi ya wafanyakazi. Mpango huu umeleta faraja kwa wafanyakazi na kuongeza ari na tija ya kazi.

### Muundo Mpya wa Utumish (Scheme of Service)

Chuo kiliboresha muundo wake wa utumishi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa malengo ya taasisi. Hadi kufikia mwezi Mei, 2024 kiasi kikubwa cha nafasi mpya zilikua zimejazwa.

National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# WATUMISHI

## Upandishaji Madaraja (Staff Promotion)

Zaidi ya wafanyakazi 50 wamepandishwa madaraja kutokana na jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu na kwa mujibu sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

## Ajira Mpya

Chuo kimeajiri wafanyakazi wapya zaidi ya 30 katika idara mbalimbali ili kuongeza ufanisi na huduma bora.

## Malipo ya EDA

Katika kipindi **hiki** Chuo kimefanya malipo ya fedha za EDA kwa watumishi wote wa Chuo ili kutoa motisha na hamasa ya kazi. hii imepelekea kuongeza ufanisi wa kazi kwa watumishi.



## MAADHIMISHO SIKU YA HUDUMA KWA MTEJA










# HUDUMA BORA

## Mkataba wa Huduma kwa Wateja (Client Service Charter)

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Chuo kilizindua mkataba mpya wa huduma kwa wateja ambao unatoa miongozo na viwango vya huduma bora kwa wanafunzi na wadau wengine wote wa Chuo.








HATI YA MASHIRIKIANO NA CHUO CHA BAHARI DAR ES SALAAM (DMI)




KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI TAALUMA (PAC)




HATI YA MASHIRIKIANO NA JESHI LA POLISI TANZANIA




HATI YA MASHIRIKIANO NA CHUO KIKUU CHA KITEKNOLOJIA CHA TSH
CHA AFRIKA KUSINI

# USHIRIKIANO WA KIMKAKATI










**Chuo kimesaini mikataba ya ushirikiano na taasisi mbalimbali ikiwemo:**

- Chuo Kikuu cha Kiteknolojia cha Tshwane (Tshwane University of Technology) - cha Afrika Kusini
- Jeshi la Polisi Tanzania
- Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI)
- Chuo Kikuu cha Umma cha Zanzibar (SUZA)
- Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu (PMO);
- CHuo Kikuu cha Teknolojia cha Vaal - Afrika Kusini
- Hospitali ya Taifa ya Muhimbili
- VETA

## TAMASHA LA VYAKULA ASILI









National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# TAMASHA LA VYAKULA VYA ASILI

Katika mwaka wa masomo 2023/24 Chuo kiliandaa tamasha la Vyakula vya asili ambalo lilishirikisha wanafunzi, wakufunzi na wadau mbalimbali. Tamasha hili lililenga kukuza utamaduni na kudumisha vyakula vya asili vya watanzania.





**Pichani**

Mkuu wa Chuo Kulia pamoja na Wakufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii walioshiriki katika tamasha hili la vyakula vya asili tanzania

# MIKUTANO YA KIMATAIFA

Katika kipindi hiki chuo kiliandaa Mkutano wa pili wa Kimataifa wa LIATH-DC uliowakutanisha pamoja Wanataaluma na Wadau katika Sekta ya Utalii. Washiriki kutoka nchi mbalimbali kama Kenya, Zambia, Afrika Kusini na Tanzania walishiriki Mkutano huu ambapo zaidi ya tafiti 35 ziliwasilishwa na kujadiliwa.

Vilevile chuo kinaendelea na maandalizi ya Mkutano wa tatu wa Kimataifa (3rd LIATH-DC) ambao unaandaliwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Tshwane (TUT) na Chuo cha Utalii Kenya (KUC) unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba 2024 wenye maudhui ya “Green and Blue Tourism Strategies Towards Sustainability and Digitalization”.



National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# HUDUMA YA CHAKULA NA VINYWAJI



- Chuo kimeanzisha huduma ya utoaji chakula katika Mji wa Kiserikaki Mtumba, jijini Dodoma, kikilenga kuboresha lishe na afya ya wakazi wa eneo hilo lakini pia kuongeza mapato ya ndani ya taasisi.



PICHA YA PAMOJA YA VIONGO WA CHUO NA WAWAKILISH WA JESHI LA POLISI BAADA YA UTIAJI SAINI HATI YA MASHIRKIANO

National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"





# UPATIKANAJI WA ARDHI

**Njombe**
Chuo kimepata ekari 25 za ardhi mkoanii Njombe kwa ajili ya upanuzi wa huduma zitolewazo na Taasisi.

**Ilemela**
Chuo kimepata hati miliki za viwanja katika Halmashauri ya MAnispaa ya Ilemela, Jijini Mwanza kwa ajili ya uendelezaji wa Kampasi ya Mwanza. Mpaka sasa Chuo kina mita za mraba **108,016** katika eneo la Shibula na mita za mraba **8,880** katika eneo la Semba


NA UMOJA

National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# MAFUNZO KWA WADAU

Katika kipindi hiki Chuo kilifanikiwa kutoa kozi fupi kwa wadau mbalimbali walio katika mnyororo wa thamani wa Utalii kama ifuatavyo:

1. Maafisa wa Polisi zaidi ya 8,130 walipatiwa mafunzo kuhusu huduma rafiki za kipolisi kwa Watalii hususan katika huduma kwa wateja, usimamizi wa utalii, na utunzaji wa muda.
2. Zaidi ya Maafisa 400 wa Idara ya Uhamiaji walipatiwa mafunzo ya huduma bora kwa wageni hususani watalii wanapoingia na kutoka nchini.
3. Mafunzo mengine yalifanywa kwa wahudumu wa ndege 10 kutoka Wakala wa Ndege za Serikali ya Tanzania (TGFA) kuanzia tarehe 28 Machi - 8 Aprili, 2024.
4. Chuo kinaendelea na utoaji wa kozi maalumu ya Wapishi wa Melini “Ship Cooks” inayotolewa kwa kushirikiana na Chuo cha Bahari cha Dar es salaam (DMI). Kozi hii ilianza kutolewa mwezi Februari 2023 na mpaka sasa jumla ya Wapishi wa Melini 28 wamehitimu kozi hiyo.
5. Pia Chuo kiliendesha mafunzo ya Huduma kwa Wateja kwa Wafanyakazi 76 kutoka Shirika la Reli Tanzania ambao wanatoa huduma katika Treni ya Mwendokasi (SGR) ikiwa ni juhudi za pamoja za taasisi zetu kuboresha huduma zinazotolewa katika Treni.







National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

# UFADHILI WA MASOMO

Zaidi ya wanafunzi 20 wamepata ufadhili wa masomo kupitia Ufadhili wa Masomo wa Pangani uliolenga kusaidia wanafunzi wenye uhitaji, wanafunzi hao wanasoma programu za utalii na za waongozaji wa watalii.





# Matumizi ya Kiteknolojia

Chuo kimepanua matumizi ya mifumo na teknolojia mbalimbali ya kidijitali katika utoaji wa mafunzo na huduma zake. Mifumo hii inajumuisha:-

### Mfumo wa Taarifa za wanafunzi (SARIS)




### Mfumo wa Hotel Reservation - OPERA




### Mfumo wa Utunzaji Machapisho ya Kitaaluma - (Repository)




Aidha Chuo kimeimarisha matumizi ya mifumo mbalimbali ya kiserikali, ikiwemo mfumo wa manunuzi serikalini (NeST), Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE), na Mfumo ya Upimaji Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS)



# MAFANIKIO MENGINE

- Ushiriki katika kampeni za utunzaji wa mazingira
- Uanzishwaji wa kituo cha ubunifu na ujasiriamali kwa Wanafunzi. Kituo hiki kitawasaidia wanafunzi na wahitimu wa Chuo kuanzisha na kusimamia biashara zao.
- Ushirikiano na sekta binafsi katika miradi ya maendeleo ya jamii










National College of Tourism
"A Ladder to Excellence"

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
CHUO CHA TAIFA CHA UTALII
SAMORA AVENUE NA SHAABAN ROBERT
S.L.P 9181 | SIMU: + 255 22 2125901/2 | +255 222125916
FAX : +25522212 5248
Website: www.nct.ac.tz | E-mail : info@nct.ac.tz | Dar es Salaam.